Nchi Yetu

# RUFIJI YETU

RUFIJI DISTRICT COUNCIL
HALMASHAURI YA WILAYA RUFIJI

26-08-2022

Www.instagram.com/rufiji_dc  https://rufijidc.go.t  www.facebook.com/rufiji.dc



Mhe. Juma A. Ligomba
Mwenyekiti wa Halmashauri



**Ndg. John L.. Kayombo**
**Mkurugenzi Mtendaji—Rufiji**

**Yaliyomo;**



| | |
|---|---|
| Habari | 2 |
| Habari | 3 |
| Habari Picha | 4 |
| Habari Picha | 4-5 |
| Miradi na Huduma | 6-7 |
| Miradi na Huduma | 8-9 |
| Matangazo | 10 |



## KAYOMBO AONYA WATAKAOBADILISHA MATUMIZI, FEDHA ZA MIRADI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji John Lipesi Kayombo amezitaka Kamati za Ujenzi zinazotekeleza miradi ya maendeleo kutobadilisha matumizi ya fedha za bakaa zinazopelekwa na kusisitiza zitumike kwa lengo lililokusudiwa.



Ameyasema hayo wakati akitoa maelekezo kwa Wakuu wa idara na vitengo katika kikao chake cha ijumaa kilichofanyika ukumbi mdogo wa Halmashauri.

***" Tuna bakaa ya Bilioni 1.3 . Yote inakwenda kwenye miradi ya maendeleo. Hakuna fedha kufanya kitu kingine."*** alisema Kayombo.

Ameongeza kuwa Halmashauri imejipanga kutatua changamoto za Wananchi wa Rufiji na kuboresha mazingira ya Wafanyakazi ili kuleta ufanisi katika uzalishaji na utendaji kazi.

***" Tuwasaidie wananchi wa Rufiji kwa kuiga mfano wa Mhe. Rais ." alisema***

Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji inatarajia kukamilisha miradi yote 152 na kuanza miradi mipya ikiwemo miradi inayolenga kuinua uchumi wa Halmashauri kwa kuongeza tija katika ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuongeza fursa za ajira kwa vijana.

## MHE. MCHENGERWA AHESABIWA.



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mbunge wa Jimbo la Rufiji Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa ameshiriki kuhesabiwa mapema Leo Agosti 23. 2022 nyumbani kwakwe Ikwiriri Wilaya ya Rufiji Mkoani Pwani.

# WENYEVITI WAPEWA MAELEKEZO

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji Meja Edward Gowele amewataka Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji kuhakikisha wanashiriki kikamilifu wakati wa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ili kuhakikisha Makarani wanapata takwimu sahihi.

Ameyasema hayo leo Agosti 21 katika kikao cha maelekezo ya utekelezaji wa zoezi la sensa kwa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji kilichofanyika katika ukumbi wa chuo cha maendeleo ya wananchi (FDC) Ikwiriri.

" lazima tutambue dhamana yetu kwenye jambo hili kwa maslahi makubwa ya Taifa. Uzalendo tuutangulize mbele." Alisema Mkuu wa Wilaya.

Aidha amewasisitiza Wenyeviti wa Vitongoji kutumia fursa hiyo, kupita maeneo yote ndani ya vitongoji vyao ili kupata taarifa halisi za watu wao kwenye maeneo yao "Kiongozi anayewajibika kwenye nafasi yake ipasavyo anamjua kila mwananchi wake na changamoto zake, tumieni fursa hiyo ya kuhakikisha mnawaongoza makarani vizuri ili nanyi mpate taarifa sahihi." Alisema. Kwa upande wake Mratibu wa Sensa Wilaya ya Rufiji Faustine Selestine ameeleza kuwa zoezi la sensa kwa upnde wa dodoso la Jamii limeanza rasmi na kuongeza kuwa kwa Wilaya ya Rufiji hakuna upungufu wa makarani wa Sensa.

" Hakuna upungufu wa makarani wilaya ya Rufiji hivyo tuhakikishe kila mmoja wetu anahesabiwa." Alisema Mratibu



*Mratibu wa sensa akitoa elimu ya sensa kwa wenyeviti(picha: habari na mawasili-*

## MAKARANI WATAKIWA KUWA WAZALENDO

Mkuu wa wilaya ya rufiji Meja Edward Gowele amewataka Makarani na Wasimamizi maudhui kuwa Wazalendo na Waaminifu ili kuiwezesha Serikali kupata takwimu sahihi.

***" hakikisha katika eneo lako aachwi mtu hata mmoja wale wote wenye changamoto wahesabiwe"*** alisema gowele

Aidha amewataka makarani hao kujihepusha na vitendo vya rushwa huku akisisitiza utunzaji wa vifaa vya Serikali walivyokabidhiwa na kuwa vinakuwa salama mda wote wa zoezi la sensa



*Mhe. Meja Edward Gowele mkuu wa wilaya akiongea na makarani wa sensa siku ya alhamisi mji wa ikwiriri.*



# MWENYEKITI WA HALMASHAURI AHESABIWA.

Mwenyekiti wa halmashauri ya wilya ya rufiji mh. Juma Ligomba ameshiriki sensa ya watu na makazi kwa kuhesabiwa nyumbani kwake nyamwage, kata ya Mbwara Wilayani Rufiji Mapema Agosti 23, 2022



## BONANZA LA UAMASISHAJI SENSA LAFANYIKA RUFIJI.

Bonanza hilo lilianza na mbio (jogging) lililoshiriki mkuu wa wilaya na viongozi mbalimbali pamoja na wananchi asubuhi saa 12 kwa mbio za mchakamchaka kuanzia ofisi ya mkuu wa wilaya kuzunguka mji na kutamatika katika viwanja vya Azimio(mabatini).



Pia michezo mbalimbali ilifanyika iliyoshirikisha viongozi na wananchi kama vile kukimbiza kuku, kuvuta kamba, mchezo wa bao, kukimbia mbio fupi,kucheza rede upande wa akina mama pamoja na mpira wa miguu uliousisha watumishi wa serikali pamoja na madiwani wa kata mbalimbali wilayani rufiji.

Sambamba na michezo hiyo mkuu wa wilaya mh. Edward Gowele amewataka wananchi kushiriki zoezi katika zoezi la sense ya watu na makazi tarehe 23/08/2022.

" suala la sense ni la kitaifa, sisi sote atuna budi kushiriki na tuakikishe watu wote wanahesabika siku ya tarehe 23/08/2022". Alisema.

Kwa upande wao Wananchi pamoja na viongozi wamekubaliana kushiriki kikamirifu katka zoezi la sensa linalotarajiwa kufanyika tarehe 23/08/2022.



# MATUKIO KATIKA PICHA BONANZA LA SENSA












# MATUKIO KATIKA PICHA BONANZA LA SENSA










# UTEKELEZAJI WA MIRADI NA HUDUMA

## SEKTA YA ELIMU:

### A) Fedha za Mapato ya Ndani (Own Source Revenues)

Katika kipindi hiki, Jumla ya kiasi cha shilingi **720,748,600** fedha za Mapato ya ndani, zimetumika katika Ujenzi na ukamilishaji wa Madarasa **22,** Nyumba ya Walimu **4**, na Matundu ya vyoo **106,** ambapo Nyumba **1**, Madarasa yote **22** na Matundu **34** yamekamilika na yanatumika. Aidha; Jumla ya Madawati **876** yametengenezwa na yanatumika.





### Fedha toka Seikali Kuu na Wahisani wa Maendeleo

Katika kipindi hiki, Sekta ya Elimu Msingi, ilipokea Jumla shilingi **457,572,379** fedha toka Serikali Kuu (Tshs. **112,500,000**), fedha toka kwa Wahisani wa Maendeleo (Tshs. **240,000,000**)**,** Mfuko wa Elimu na P4R ni **(**Tshs**. 105,072,379)** na jumla ya Matundu **14** ya vyoo na Madarasa **28** yamejengwa, ambapo madarasa **21** na Matundu yote **14** ya vyoo yamekamilika na yanatumika.





# UTEKELEZAJI WA MIRADI NA HUDUMA

### B)SEKTA YA ELIMU SEKONDARI

### Fedha za Mapato ya Ndani (Own Source Revenues)

Katika Sekta ya Elimu Sekondari, Jumla ya kiasi cha shilingi **870,000,000** fedha za Mapato ya ndani, zimetumika katika Ujenzi na ukamilishaji wa Madarasa **43** na Mabweni 3 katika Shule za Sekondari **Kazamoyo**, **Mohoro**, na **Ngorongo**. Aidha**;** Madarasa **35** na Mabweni yote **3** yamekamilika na yanatumika, na Madarasa **8** yapo hatua za mwisho za Ukamilishaji.





### Fedha toka Seikali Kuu na Wahisani wa Maendeleo

Katika kipindi, Halmashauri ilipokea Jumla ya kiasi cha shilingi **5,224,047,403** fedha toka Serikali Kuu **(**Tshs. **262,500,000),** fedha toka kwa Wahisani wa Maendeleo (**SEQUIP**) (Tshs. **3,940,000,000**), na P4R ni **(**Tshs**. 151,872,373),** fedha za UVIKO/IMF **(**Tshs**. 720,000,000)** na TASAF (Tshs. **149,675,030**) kwa ajili ya Ujenzi wa Shule Mpya 2 za Sekondari katika Kata za Ngarambe na Ngorongo, Shule Maalum ya Wasichana shule ya sekondari Bibi Titi Mohamedi, Ujenzi wa Madarasa **42** na Mtundu ya vyoo **8** na Bwalo la chakula katika Shule ya Sekondari Mohoro. Aidha; mpaka mwaka wa fedha unaisha Juni 30, 2022 Jumla ya Madarasa **42** yamejengwa na kukamilika na Ujenzi wa hizi shule mpya upo hatua mbalimbali za Utekelezaji.







# UTEKELEZAJI WA MIRADI NA HUDUMA

## SEKTA YA AFYA

### Fedha za Mapato ya Ndani (Own Source Revenues)

Katika Sekta ya Afya, tumeendelea na uboreshaji wa Miundombinu ambapo kwa kipindi cha Mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya kiasi cha Tshs. **472,000,000** fedha toka Mapato ya ndani, kilielekezwa katika Sekta ya Afya kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati Mpya **6** (Katundu, Nyawanje, Umwe Kusini, Mgomba Kusini, Ngorongo Magharibi, na Msona), Ujenzi wa Jengo la Mionzi (Hospitali ya Utete), na Ununuzi wa dawa na vifaa tiba. Aidha; Utekelezaji wa Ujenzi wa Majengo haya, upo hatua mbalimbali za Umaliziaji.



### (b) Fedha toka Serikali Kuu

Katika Kipindi hiki pia, Halmashauri ilipokea kiasi cha shilingi **1,890,000,000** fedha toka Serikali Kuu ( Tshs. **500,000,000**), Tozo ya Miamala ya Simu (Tshs. **1,000,000,000**), na fedha za UVIKO/IMF ni (Tshs. **390,000,000**). Fedha hizi ni kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ifuatayo:-

- Ujenzi wa Vituo cha Afya 2 vya Ngorongo na Ngarambe (Jengo la Mama na Mtoto, OPD, Maabara, Mfumo wa Maji Taka, Jengo la Upasuaji)
- Upanuzi wa Zahanati ya Mkongo kuwa Kituo cha Afya, Ujenzi wa Jengo la Maabara Kituo cha Afya Mloka, umaliziaji wa Ujenzi wa nyumba 2 za Watumishi (Zahanati ya Ndundutawa na Nyamakurukuru)
- Ujenzi wa jengo la huduma za dharula katika kituo cha afya Ikwiriri

Ujenzi wa nyumba moja (3 in 1) ya watumishi katika kituo cha Afya Ngorongo.
Ujenzi Unaendelea, na majengo yapo hatua mbalimbali za Utekelezaji.







# UTEKELEZAJI WA MIRADI NA HUDUMA



## RUFIJI YETU

Halmashauri ya wilaya ya rufiji
S.l.p 28,
Utete/rufiji.

TEL: +255232010304
FAX: +255232010317
Email: ded.rufiji@pwani.go.tz

